

Utawala wa Mreno unazidi kunuka

UKOLONI wa Mreno unatia fora...Licha ya ubaguzi na kunyimwa elimu kwa Waafrika huko, lakini pia ule utumwa wa kufanyishwa kazi kwa nguvu.

Haya ni malalamiko yaliyotolewa jana na chama cha FLERIMO kilicho na makao yake makuu hapa DSM kwa ajili ya wakimbizi toka pande hizo.

"Jitihada za watu wa Msumbiji kutaka uhuru kwa njia za amani zimeshindwa kufaulu." Taarifa ilizidi kusikitika. 'Utawala huo ahalimu umeshindwa kuheshimu juhudi za Jumua ya Madola kuta kanchi hiyo ipate uhuru wake.

Hawezi

Taarifa hiyo ilizidi kuyasusa mataifa ya Magharibi katika

ushirika wa NATC 'Hayam', ilinena taarifa, ndiyo yanayohusika katika kumwuzia silaha Mreno. Mataifa hayo kama hayangalitoa msaada wa silaha ama misaada ya fedha, Mreno hangaliweza kuishi.

Kwa kumaliza taarifa mwandishi alikumbusha mauaji ya juzi ya watu wawili ambao walipigwa risasi walipoonwa na polisi wakisoma barua kutoka Tanganyika. Kulikuwa hakuna swali bali askari alifyatua bunduki na kuwaua watu hao. Wengine wawili ambao waliumia wanasadikiwa kuwa wamefariki katika jela la askari washenzi wa Mreno.